Kikao cha Tano – Tarehe 19 Oktoba, 2011

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahamoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 13

Ujenzi wa Msikiti Katika Baraza la Wawakilishi

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Bismillah Rahman Rahim. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti kwa sababu hili ni suala la duni ndio nikaanza kwa *Bismillah.* Kwa ruhusa yako naomba nijibiwe kama nilivyouliza, ahsante.

Tatizo kubwa tulilonalo hapa Baraza la Wawakilishi ni sehemu ya kufanyia ibada ya sala. Waheshimiwa Wajumbe na Watendaji wa Serikali hulazimika kusali nje ya Jengo la Baraza la Wawakilishi jambo ambalo halifanani kutokana na hadhi ya Jengo la Baraza la Wawakilishi lilivyo.

Wizara ina mpango gani hasa wa kuona kuwa Msikiti unajengwa katika eneo hili la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Bismillah Rahman Rahim. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Mjumbe swali Nam. 13 kama ifuatavyo kwa ufanisi mkubwa:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa hivi sasa kuna tatizo la kutokuwepo kwa sehemu rasmi ya kusalia ndani ya eneo letu la Baraza hapa Chukwani. Hali hiyo imekuwa ikileta usumbufu kwa Waheshimiwa Wajumbe, Watumishi wa Baraza na Watendaji wa serikali wanaokuja kuhudhuria kwenye vikao vya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, makisio ya awali yalifanywa pamoja na michoro ya ujenzi wa Msikiti na ilikisiwa kwamba ujenzi ungegharimu Shilingi Milioni 75, Sabiini na Tano. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 ujenzi wa Msikiti haukutengewa fedha kwenye bajeti ya Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, jitihada zimefanywa kutafuta wafadhili wa kusaidia ujenzi wa Msikiti huo. Tayari kuna mfadhili mmoja ameonesha nia ya kusaidia ujenzi huo, lakini ametuomba tufanye subra kidogo, ili aweze kujipanga vizuri na kujiandaa kwa ajili ya kusaidia katika ujenzi huo wa Msikiti.

Halikadhalika, tuliwaomba waumini ambao ni wadau wakubwa wa msikiti huo unaotaka kujengwa nao pia wachangie. Waumini hao ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Watumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nina furaha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wamechangia Shilingi milioni 4,850,000/= na kwa upande wa Watumishi wa Baraza, nao wamechangia Shilingi 4,385,000/=. Jumla ya michango hiyo imefikia Shilingi milioni 9,235,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mfadhili tunaemtegemea bado hajawa tayari na kwa kuwa ujenzi wa Msikiti ni jambo lenye thawabu nyingi na ni sadakat-Jariyah, hivyo tutaendelea kuwasiliana na wafadhili wengine, ili tuweze kupata michango zaidi kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, takriban sote ni Waislamu na tunajua umuhimu wa swala. Mahala pa kuswalia ni lazima pawe safi, vifaa vya kusalia viwe safi na kadhalika. Leo tunasali nje, matope ya gari yanapita pale pale, ndege wanakunya pale pale na kadhalika. Sisi ni kuweka majamvi na kuondoa ambapo sio utaratibu.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wajumbe wako wa Baraza hili na watendaji wameshaonesha juhudi yao ya kutoa mchango na kwa sababu yuko mfadhili kajitokeza tu, lakini bado hajaanza na Mhe. Waziri hakueleza ni lini suala hili labda litaanza kufanikiwa.

Je, wizara haiwezi kufanya mpango wa kutafuta wafadhili wengine wa humu ndani, ili kuona suala hili linaanza japo hatua kwa hatua, badala ya kungojea msaada wa pamoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, serikali na sote tunafahamu umuhimu wa ibada hii tukufu ya swala na umuhimu wa swala yenyewe kufanyika katika pahala pasafi, na ndio maana jitihada zinafanywa ili tuweze kupata michango na kuweza kuwa na Msikiti wetu katika Baraza letu hili tukufu. Kwa kuwa mwaka huu wa fedha serikali haikutenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo, lakini tuna matumaini kwamba mwaka ujao jitihada hizo zitaendelezwa na kwa sasa ushauri wa Mhe. Salum Abdalla na sisi wenyewe tutaendelea kama nilivyosema katika jibu langu la

msingi, kuweza kuwasiliana na wafadhili mbali mbali ili watusaidie katika ujenzi huo. Naamini watajitokeza kwa kuwa ni jambo la kheri.

Hata hivyo, juu ya msaada mkubwa ambao Waheshimiwa Wajumbe wameonesha, basi naamini kuwa wapo wengine ambao na wao tayari wameonesha nia ya kuchangia zaidi. Kwa hivyo, inawezekana kabisa pengine wakatokea waheshimiwa wenyewe humu ndani wakaweza kulimalizia suala hili bila ya kupata mfadhili kutoka nje. Naamini Mhe. Salim Abdalla naye ameonesha nia hiyo, kwa kiasi atakachoweza basi tutaendelea kukushukuru, ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa Msikiti siku zote humsubiri muumini kufanya ibada zake, lakini ibada siku zote haimsubiri muumini na muumini hutakiwa kuabudu angalau mara tano kwa siku. Kwa sababu sehemu tunayofanyia ibada hairidhishi kama alivyouliza mwenye swali la msingi.

Je, ni lini pamoja na uwezo mdogo tulionao kuweza kuwekewa *temporary shelter* pale ambayo itakuwa haipiti magari, kusudi kuweza kufanya ibada zetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tutajitahidi kushirikiana na uongozi wa Baraza, ili tuhakikishe kwamba wajumbe wa Baraza hili tukufu na viongozi mbali mbali wanaokuja katika ukumbi huu na wananchi waweze kupata eneo zuri na lililosafi kwa ajili ya sala. Tutachukua jitihada hizo ili kuhakikisha kwamba sala inafanyika katika mazingira yaliyo mazuri na safi.

Nam. 85

Upelekaji wa Mahabusu Mahakamani

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Jambo zuri linafaa kuigwa. Kule Bara uchukuaji wa Mahabusu kwenda Mahakamani unafanywa na Magereza. Hapa kwetu hadi hii leo bado linashughulikiwa na Polisi. Pia usafiri wenyewe ni wa hatari kwani hakuna lile gari maalum la kuchukulia mahabusu. Kule Pemba kwa mara nyingi zinatumika gari za Wakuu wa Polisi Wilaya OCD.

Mhe. Waziri huoni kuwa kuna haja kwa hapa Zanzibar kazi hii wakaachiwa Askari wa Mafunzo na wakatafutiwa magari ya kisasa ya kubebea mahabusu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake 85 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba jambo zuri linafaa kuigwa. Nakiri kwamba ni kweli kule Bara wenzetu wanachukua mahabusu kwenda mahakamani na watu wa magereza. Lakini zoezi hili la kuwapeleka na kuwarejesha mahakamani mahabusu linafanywa na askari wa magereza kwa Mkoa wa Dar es Salaam tu peke yake, ambapo jeshi la magereza liliopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Tanzania, wizara ambayo ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na jeshi la magereza pamoja na jeshi la polisi. Napenda niwafahamishe kwamba zoezi hilo ni la majaribio tu na wizara imeamua lifanywe kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, yapo magari maalum makubwa kama alivyosema Mhe. Mwakilishi, ambayo kazi yake ni kusafirisha mahabusu kwa wingi wake. Kwa mfano hapa Mjini Unguja lipo gari moja kubwa kabisa karandinga lile ambalo wanachukuliwa mule. Lakini kwa miji midogo au sehemu zenye mahabusu kidogo basi gari lile halipo, lakini panapaswa pawepo gari nyengine ndogo yenye usalama mzuri ambao wanaweza kuingia mahabusu na askari wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakiri kwamba Pemba gari hizo ndogo hakuna, lakini tutawasiliana na wenzetu wa polisi ili ziweze kupatikana gari hizo ndogo ili ufanisi wa kazi hiyo uweze kupatikana. Ahsante sana.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Je, Mhe. Waziri hizi ni gari za aina gani zinazotakiwa kusafirishia mahabusu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nielezee kwamba mahabusu bado hawajawa wafungwa, kwa hapa kwetu tunasema bado hawajawa wanafunzi. Yaani kwa Kizungu tunasema wao ni *unconverted prison*, yaani bado hawajafungwa. Kwa mantiki hiyo bado wanakuwa chini ya polisi.

Kwa hivyo, gari wanalopaswa kuchukua ni gari ambalo lina usalama, namaanisha kwamba wanaposafirishwa wasiweze kutoroka, kwa sababu unajua bado kama nilivyosemwa hawajatiwa hatiani, basi inabidi ulinzi wao uwe mzuri zaidi. Hata kama wameshatiwa hatiani. Kwa hivyo, ni gari yenye usalama na pia kuwatenganisha kati ya askari wanaowachukua na hao mahabusu wenyewe. Mnajua mara nyingi wengine huweza kupata nafasi ya kukimbia au wakafanya madhara hata kwa askari. Kwa hivyo, gari lihakikiswe lina usalama mzuri. Kama gari lina usalama mzuri basi hata wakati mwengine kama gari za wakuu wa polisi wa wilaya huazimwa kwa kazi hiyo, kwa ukosefu wa hilo gari lenyewe. Lakini lengo letu tutafute gari lenyewe na utayaona magari yenyewe yana waya ambayo yanatenganisha kati ya mahabusu, dereva na askari wake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali ya tatizo la usafiri wa mahabusu ambao hauendani na mazingira ya sasa, lakini pia kuna tatizo jengine linalowakabili

mahabusu ni maeneo yale wanayowekwa katika magereza yetu hasa magereza mawili, gereza la hapa Kiinua Miguu na la Wete ambayo yanaonekana yana mrundikano mkubwa sana, kiasi cha kuwasababishia matatizo makubwa, mbali ya huduma ambazo zimo katika magereza haya.

Mhe. Mwenyekiti, sijui wizara yake imejipanga kiasi gani kuona mbali suala hilo la usafiri lakini kwa jumla inazingatia mambo haya na kuifanya Zanzibar iingie katika zile nchi ambazo zinazingatia misingi ya haki za binadamu katika kuwashughulikia watu wa aina hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ingawa swali limegusa usafiri wa mahabusu na Mhe. Ismail Jussa ameulizia mazingira ya mahabusu. Hata hivyo, nitajaribu kumjibu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi mimi mwenyewe nilitembelea Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo na kwa kweli nimeridhika na hali niliyoiona ndani na mahabusu, nakiri kwamba wapo wengi na kama nilivyosema kuwa bado kesi zao ziko mahakamani. Lakini hali iliopo ni nzuri, tumetembelea mpaka jikoni, malazini kwa kweli kunaridhisha kabisa. Namuomba Mhe. Ismail Jussa kama yeye yuko tayari kama mwakilishi na mtetezi wa haki za binadamu, basi twende pamoja tukaione hiyo hali, hali sio mbaya tumeendelea sana kwa kweli na tunavyowajali mahabusu wetu.

Nam. 69

Wanafunzi wa Chuo cha Uongozi wa Fedha Kutumia Majengo ya Glorious Academy – Mpendae

Mhe. Mohammed Said Mohammed - Aliuliza:-

Wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Diploma ya '*Procurement*" wa Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka wanayatumia majengo ya skuli ya "*Glorious Academy*' iliopo Mpendae katika kufundishiwa, badala ya wanafunzi hao kufundishia kupitia Majengo ya Chuo cha Uongozi wa Fedha yaliyopo Chwaka.

(a) Je, kuna sababu gani za msingi za wanafunzi hao kutumia majengo ya mtu binafsi.

(b) Je, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka kimekodi majengo ya skuli "*Glorious Academy*".

(c) Na kama ndio, je kuna Mkataba wa ukodishwaji huo na ni kiasi gani Chuo cha Uongozi wa Fedha hulazimika kumlipa mmiliki wa '*Glorious Academy'* kwa mwaka.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo -Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la lake nambari 69, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, kilianza kutoa mafunzo ya kada ya uongozi wa fedha kwa kiwango cha cheti tokea mwaka 1999, kikiwa na wanafunzi 32 na darasa moja tu. Kutokana na mahitaji ya wataalamu wa kada mbali mbali kama vile uhasibu, fedha, benki, ugavi na manunuzi. Chuo kililazimka kusajili wanafunzi zaidi na kuongeza aina ya mafunzo mwaka hadi mwaka, kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya mbali mbali ya wataalamu wa kada hizo hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kasi ya mahitaji ya kusomesha wataalamu wa kada hizo, zilikuwa haziendi sambasamba na kasi ya kuongezeka kwa miundombinu ya kuwahudumia wanafunzi hao. Miundombinu hiyo ni pamoja na madarasa, dakhalia na gari kwa ajili ya usafiri wa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa utawala. Idadi ya wanafunzi waliosajiliwa chuoni iliongezeka mwaka hadi mwaka, kutoka wanafunzi 30 mwaka 1999/2000 kwa ngazi ya cheti hadi kufikia wanafunzi 850 mwaka 2010/2011 katika taaluma na viongo tofauti hadi kiwango cha shahada.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na idadi kubwa ya vijana walioomba yanayotolewa na Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, chuo kililazimika kutafuta njia mbadala zitakazo wezesha kumudu changamoto iliyojitokza, ili wanafunzi hao ambao baadae watakuwa tegemeo kwa maendeleo ya taifa letu wapate nafasi ya masomo kwa kada walizoomba, badala ya kuwaacha kwenda kutafuta masomo katika vyuo viliopo nje ya Zanzibar ambavyo vina gharama kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 69 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, sababu ya msingi ilopelekea Chuo cha Uongonzi wa Fedha Chwaka, kutumia majengo ya mtu binafsi ni kutokana na chuo kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi, ikilinganishwa na uwezo wa miundombinu, ikiwemo huduma za dakhalia pamoja na mabasi kwa ajili ya usafiri wa wanafunzi na walimu.

   Aidha, chuo kililazimika kutumia madarasa hayo kwa vile yana kiwango kinachokubalika na matakwa ya wasimamizi wa vyuo vya ufundi Tanzania, yaani *National Council for Technical Education*. Kwa kifupi (*NACTE),* baada ya kushindwa kupata madarasa yenye sifa hizo kutoka katika taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(b na c) Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, kimekodi ghorofa ya tatu ya ya jingo la skuli ya *Glorious Academy,* pamoja na huduma za viti, meza na *Computer* kwa mkataba wa muda wa mwaka mmoja, kwa matumizi kuanzia saa 1:00 za asubuhi mpaka usiku kwa siku zote za wiki.

Malipo kwa mwaka ni Shs. 26,000,000/= ambapo ni sawa na wastani wa Shs. 2,160,000/= kwa mwezi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya kwa urefu kabisa ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kukodi majengo mjini baada ya kukodi karibu na *campus* yenyewe ili kuleta uhalisia wa chuo halisi.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba hukodi tu jengo, bali unakodi jengo ambalo lina sifa zinazotakiwa na *NACTE*. Katika eneo la Chwaka hakuna jengo ambalo lina sifa zinazotakiwa na *NACTE.* Hata hivyo, tungeweza tukakodi jengo kama lingekuwa lina sifa katika maeneo ya Chwaka, lakini bado tungelazimika kutafuta usafiri au hao wanafunzi kujitegemea kwa kutoka mjini kwenda Chwaka na kurudi mjini, ni zaidi ya Shs. 2600/=.

Mhe. Mwenyekiti, la msingi ni kwamba chuo hiki tukiwezeshe kuwa na majengo zaidi, madarasa, madakhalia pamoja na usafiri ili hawa wanafunzi waendelee kukaa pale, ili tuweze kuwapunguzia gharama za kusoma.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Je, anaweza kulitajia Baraza lako tukufu ni nani mmiliki wa Skuli ya *Glorious Academy* ambayo Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imekodi kwake majengo hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Hajasikia rudia tena. Uliza taratibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namuuliza taratibu, mpiga kura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe. Mhe. Waziri swali langu ni kwamba je, unaweza kulitajia Baraza la Wawakilishi ni nani mmiliki wa majengo ya *Glorious Academy* ambayo Wizara yako ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imekodi kwa ajili ya matumizi haya kutoka kwake.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sio wizara ambayo iliyokodi hilo jengo, nataka niweke usahihi kabisa. Chuo kile cha Chwaka kina uongozi na ndio ambao umekodi hilo jengo.

Pili, ameomba nimwambie mmiliki wa majengo hayo ya *Glorious Academy*, hivi sasa hapa sina jina, lakini namuomba anipe muda nitamtafutia na nitampa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa sababu jina bahati mbaya hajalipata, lakini atalitafuta. Naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwenye kasma ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo Baraza hili lilipitisha ruzuku ya Chuo cha Fedha Chwaka.

(a) Je, anaweza akatuambia kwamba Baraza hili lilipitisha fungu hilo kwa ajili ya kukodi jengo la chuo hicho au ruzuku ile ilikuwa ni kwa ajili ya masomo na huduma za wanafunzi.

(b) Kwa nini mkaamua kwenda *Glorious Academy* kukodi na msiamuwe kukodi majengo ya kisasa mazuri Mombasa maarufu kwa jina la SHAA.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, zipo taasisi nyingi za serikali tunazipa ruzuku, jinsi watakavyotumia ruzuku hiyo inatokana na mipangilio yao. Wanaweza kutumia ruzuku hiyo kwa ajili ya kufundishia, wanaweza kutumia ruzuku hiyo kwa ajili ya kulipia mishahara, wanaweza kutumia ruzuku hiyo kwa ajili ya maendeleo na kadhalika. Lakini ni kwa makubaliano baina ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na taasisi tunazozipa ruzuku.

(b) Mhe. Mwenyekiti, huu ukodishwaji una historia ndefu sana, tungependa sana sisi tupate majengo ambayo hayana gharama. Lakini kama nilivyosema kuna sifa ambazo unazitafuta, sijui Mhe. Hija Hassan Hija jengo gani alilolisema hilo la Mombasa kama lina nafasi. Inawezekana ikawa ni jengo zuri na mimi sina haja ya kukataa kwamba sio jengo zuri, lakini inawezekana kwamba hawana nafasi. Sasa utakapokwenda wakakuambia sisi hatuna nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyokwenda katika Skuli ya Haile Sellassie, tumepewa darasa moja na sisi tunataka mawili, wakatuambia hatuna nafasi, hatuna ujanja. Kwa hivyo, inabiditutafute maeneo ambayo yana nafasi. Serikali kukodi majengo ya watu binafsi sio mara ya kwanza. Tumeshakodi Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto jengo la mtu binafsi. Leo tumekodi Pemba Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora jengo la mtu binafsi, Chuo cha Utumishi kimekodi jengo la mtu binafsi, hii sio hoja kubwa sana, tunafanya lakini tunafanya kwa mikataba na kwa kipindi mpaka pale tutakapokuwa na uwezo wa kuwa na majengo yetu wenyewe.

Nam. 62

Majengo ya Mahkama

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa tokea Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Serikali haijafikiria kujenga majengo ya Mahkama. Majengo mengi ya Mahkama zetu ni ya kurithi tokea ukoloni, kuanzia Jengo la Mahkama Kuu ya Zanzibar, Mkoa na Wilaya ya Mjini.

Mhe. Waziri huoni kuwa kuna haja ya kwenda na wakati kwa kujenga majengo ya kisasa ya Mahkama kama tunavyojitahidi kujenga majengo ya kisasa ya makaazi ya watu binafsi na hata baadhi ya taasisi za umma.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na nakubalaina na Mhe. Mwakilishi kuwa kuna haja kubwa ya kwenda na wakati kwa kuwa na majengo mapya ya Mahkama.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa Mahkama hizo kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba ni mkubwa sana, na gharama zake kwa serikali peke yake hatuziwezi. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imelipa kipaumbele suala la majengo ya Mahkama, ambapo jengo moja jipya la Mahkama ya Mwera limejengwa, matano yanafanyiwa ukarabati ambayo ni Mahkama ya Chake Chake, Mkoani, Konde, Chwaka na Jengo la Mahkama Kuu Vuga. Hadi sasa kiasi cha Shillingi 981,121,800/= zimeshatumika kwa kazi hiyo, fedha ambazo zote zinatoka serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, tumejitahidi sana kutafuta wahisani ili watusaidie kujenga Mahkama zetu. Mimi binafsi nimeshzungumza na wahisani wawili kwa wakati tofauti, ili watusaidie kwa kutujengea Mahkama zetu. Hata jana Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mazungumzo na Ujumbe wa Finland, na suala hili pia nililigusia katika mazungumzo yetu, lakini bado. Utaratibu wao ni kuwa kwa fedha za kujengea Mahkama, wao huwa hawatoi. Kwa maana hiyo ni lazima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ijigharimie wenyewe katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika rasimu ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, matatizo ya Mahkama yamezingatiwa kwa kina. Vile vile tunayo mipango ya muda mrefu ambapo tunatarajia kutayarisha waraka wa mapitio wa sekta ya sheria, ambapo matatizo ya Mahkama na vyombo vyengine vya sheria yatachambuliwa na kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu. Haya ni pamoja na kuzikarabati mahakama zetu moja baada ya moja kama tunavyofanya hivi sasa na kwa kadiri ya fedha zinavyopatikana.

Nam. 37

Elimu ya Usalama kwa Wananchi Wanaosafiri

Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Kutokana na ajali zinazojitokeza na hasa ajali ya Septemba 10 mwaka 2011 ya meli *MV. Spice Islanders I,* serikali inahitaji kutoa elimu ya usalama wa usafiri kwa wananchi wake.

Je, serikali ina mpango gani juu ya suali hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 37 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba serikali inahitajika kutoa elimu ya usalama wa usafiri kwa wananchi wake. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanza kutoa mafunzo ya usalama kwa wananchi kwa kuwataka kutoa ripoti kwa tukio lolote ambalo si la kawaida katika vyombo vya usafiri na hasa vyombo vya baharini popote vilipo.

Pia Mamlaka ya Usafiri imewataka wananchi wanaponunua tiketi kuonesha kitambulisho na kuhakikisha kuwa jina la msafiri limeandikwa kwa ukamilifu katika karatasi ya *manifesto*. Sambamba na hilo mamlaka imewataka wananchi kuhakikisha kwamba tiketi wanazozinunua wanazinunua katika ofisi husika badala ya kununua mikononi, ili kuepuka walanguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri Baharini imo katika harakati za mwisho za maandalizi ya Kanuni, ili kuweza kutoa utaratibu mzuri katika masuala ya usalama baharini na taarifa pamoja na elimu kupitia vyombo vya habari.

Hata hivyo, mamlaka inawaomba wananchi, wasafiri pamoja na watumiaji wa vyombo vya usafiri wa baharini kujenga utamaduni wa kusikiliza taarifa sahihi za Utabiri wa Hali ya Hewa, ili kutambua matarajio ya hali halisi kwa siku husika.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yetu kwamba tutakapoanza kutoa elimu husika ya usalama, basi wananchi wetu watapata muamko mkubwa na kujenga taswira mpya ya ufahamu kuhusu masuala ya usalama baharini.

Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba mbali na elimu ambayo amesema ataitoa, lakini kuna matatizo ya kununua tiketi za majina ya watu wengi ambao wameaghirisha safari. Kwa hivyo, huoni kuwa hili pia ni tatizo la kuipata takwimu sahihi?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tulichokieleza ni kwamba Wizara ya Miundombinu kwa kupitia mamlaka husika tuko katika harakati za kuandaa Kanuni. Sasa kabla ya kuandaa kanuni, basi mamlaka imetoa taarifa na pia inaendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu kujenga utamaduni wa kununua tiketi katika vibanda au ofisi husika badala ya kununua mikononi, ili kuepusha ulanguzi pamoja na haya anayolalamikia Mhe. Mwakilishi ya kununua tiketi ya mtu ambaye alikuwa asafiri jana au leo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa swali lililojibiwa sana ni tiketi, basi napenda swali langu la nyongeza li-*base* hapo. Hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa kuna wauzaji wengi wa tiketi kwa shirika au chombo kimoja.

Hivi ni utaratibu gani katika kanuni hizo iliochukuliwa, ili uhakikishe kwamba tiketi zinazouzwa kwa chombo kile tena kwa safari ile ndizo zinazotakiwa ziingie kwenye chombo kile, kwa sababu wengi wanaonadisha tiketi wanauza bila ya kiwango na watu wanakwenda kukutana pwani. Kwa hivyo, inawezekana mtu hataki kusafiri na chombo kile kwa ujazo ule, lakini ameuziwa tiketi kupitia *agent* anayeuza tiketi.

(a) Je, kwenye kanuni hizo ni utaratibu gani utakaotumika, ili kuhakikisha kwamba tiketi zilizouzwa ndio uwezo wa chombo?

(b) Ni uangalizi gani uliopangwa kwenye kanuni hizo kuhakikisha kwamba wale wanaouza tiketi wanaandika majina matatu na sio jina moja kama wanavyofanya hivi sasa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Mategemeo yetu ni kwamba tutakapoweza kuzikamilisha kanuni hizi, basi utaratibu wa kuuza tiketi utakuwa unaendana na *serial number*, kwa maana ya kwamba chombo chenye uwezo wa kuchukua watu 200 basi tiketi zitaanza namba 1 hadi 200. Kutokana na hali hii, hakutokuwa na sababu ya kuuza tiketi ambazo zitakuwa zaidi ya uwezo wa chombo husika.

(b) Utaratibu kwa msafiri yeyote anaposafiri anatakiwa kuandikwa majina matatu na kama mtu atakuwa ameandikwa jina moja, basi hakuandikwa kwa ukamilifu na hivyo ni kinyume na utaratibu wa usafiri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha katika hali ya salama na afya njema asubuhi hii. Sasa naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri utakubaliana nami sasa kwamba tubadilike, kwa sababu imefika wakati wa kutumia *computer* kwa mambo yetu kama haya ya kuorodhesha majina, kwa ajili ya kupata takwimu sahihi ya wasafiri wanaosafiri?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana napenda nikiri kwamba wakati umefika wa kutumia utaratibu wa *computer*. Lakini kama tunavyotambua kwamba bado maendeleo haya yana changamoto zaidi.

Kwa hivyo, ni vyema tuangalie vizuri na tusijekuharakisha kuingia kwenye *computer* na kulazimisha huko, kwani athari za *computer* zinaweza kutusababishia usumbufu mkubwa kwa wananchi wetu wakati wanapohitaji kusafiri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wizara hatuna pingamizi na tunayaona baadhi ya makampuni tayari yameshaanza utaratibu huo kama vile Kampuni ya *Azam Marine*. Kwa hiyo, nadhani kampuni nyengine zitafuata wigo huu na wala si vibaya kuiga jambo jema na kutumia utaratibu wa *computer*.

Nam. 34

Kucheleweshwa Kuingizwa Fedha Vyuo Vikuu

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Pamoja na ahadi nyingi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika Baraza la Wawakilishi, bado kumekuwa na matatizo makubwa ya uingizwaji wa fedha kwa wanafunzi wa Zanzibar wanaosoma katika vyuo vikuu na taasisi nyengine za elimu ya juu ndani na nje ya nchi, ambao wameidhinishwa kupewa mkopo kupitia Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar, hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwao na kuwanyima utulivu wakati wanaendelea na masomo.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea wizara kushindwa kuwaingizia fedha wanafunzi hao kwa wakati?

(b) Tatizo hilo litamalizika lini?

(c) Hatua gani za haraka zitachukuliwa, ili kuwaondoshea usumbufu huo wanafunzi wanaoendelea na masomo vyuoni hivi sasa, ambao wanasumbuliwa katika kipindi hiki cha usajili wa mwaka mpya wa masomo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 34 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utanguliza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wanafunzi wetu walioko katika Taasisi ya Elimu ya Juu, ambao wamekuwa wakipatiwa Mikopo ya Masomo ya Elimu ya Juu wamekuwa hawapati fedha za mkopo kwa wakati na wengine wamekuwa wakipata usufumbu wa kuchelewa kuingiziwa fedha.

Kwa kweli usufumbu huo unatokana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutokuingiziwa fedha za kutosha kwa wakati na hivyo, hushindwa kuwalipia wanafunzi fedha za ada, chakula pamoja na malazi kwa wakati.

Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imepatiwa jumla ya shilingi bilioni 1,202,849,475/= kwa kipindi cha miezi minne ya mwanzo. Fedha hizi ni chache ukilinganisha na idadi ya wanafunzi 1022 walioko masomoni hivi sasa na wanafunzi 191 tunaowatarajia kuwapeleka.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kujibu swali la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Kuchelewa kuwapatia wanafunzi fedha za mikopo yao kwa wakati kunatokana na mambo makuu mawili.

(i) Kutokuingiziwa fedha za bajeti kwa wakati na za kutosha.
(ii) Fedha hizi zilitengwa katika bajeti yetu ni chache ukilinganisha na idadi kubwa ya wanafunzi walioko vyuoni. Pamoja na tatizo hilo Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inajitahidi sana kuingiza fedha kila hali ya ukusanyaji wa fedha inaporuhusu. *(Makofi)*

(b) Wizara inakusudia kumaliza tatizo hili hatua kwa hatua kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi kwa mujibu wa uwezo wetu. Kufanya hivyo kutawezesha kuwahudumia wanafunzi wetu vizuri tena kwa uhakika.

Vile vile wizara inatafuta vianzio vyengine vya kupata fedha kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi badala ya kutegemea fedha zinazotolewa na serikali kama ruzuku peke yake. Wizara inakusudia kufanya mazungumzo na vyombo vya fedha na kuona ni jinsi gani vitakavyoweza kutoa mikopo kwa gharama nafuu hasa kwa wafanyakazi ambao wanapitisha mishahara yao katika mabenki.

(c) Hivi karibuni wizara imeingiziwa jumla ya shilingi bilioni 725,000,000/= kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi. Fedha hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza madeni pamoja na kulipia ada za masomo. Kwa hivyo, tunawaomba wazee watekeleze pia wajibu wao kwa kuwahudumia watoto wao kwa malazi na chakula. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti pia namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba matatizo haya kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na wizara kupeleka idadi kubwa ya wanafunzi, kuliko ile ambayo imeruhusiwa au uwezo wake na ndio matokeo yake inashindwa kuwahudumia. Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kunithibitishia hilo?

(b) Katika uteuzi uliofanywa hivi karibuni wa wanafunzi wapya ambao watapatiwa mikopo. Kuna taarifa kwamba wengi waliofaidika ni wanafunzi ambao wazee wao wanao uwezo wakiwemo watoto wa vigogo badala ya wale watoto wa kimasikini.

Je, wizara itakubali Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza hili, kuchunguza mgao wa mikopo hii kwa wanafunzi hawa, ili kujiridhisha kwamba hakukupita kitu ambacho hakikubaliki katika utaratibu wetu wa kisheria?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Nataka nikiri kwamba ni kweli kipindi ambacho kilichopita tulipeleka wanafunzi wengi vyuoni zaidi ya uwezo wetu ambao tulikuwa tunao kwenye bajeti na tulipeleka wanafunzi 653. Kutokana na hali hiyo, ndio maana Mhe. Mwenyekiti tumejifunza kwa matatizo ambayo tumeyapata katika kipindi hiki, yaani tumekuwa na hali ngumu ya kukidhi mahitaji ya wanafunzi wetu walioko vyuoni. Kwa hivyo, hilo nataka nikiri kwamba ni kweli wizara ilifanya makosa hayo, tumeyaona na tumejirekebisha.

(b) Mhe. Mjumbe alisema kama kuna tetesi ya kuwa kama hao wanafunzi 191, ambao mara hii tunatarajia kuwapatia mkopo, kama mkopo huo umetolewa kiupendeleo au labda kirushwa kwa mujibu ambavyo nimemfahamu. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nataka niseme kitu kimoja kwanza, waombaji ambao waliomba ni 1603 na waliopata mkopo huu ni 191. Kwa kweli kwa horo ya kibinadamu kwa mtu yeyote yule, basi anaweza kufikiria kama hawa 191 labda kuna ghilba yoyote ambayo imetokea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba kulikuwa na vigezo ambavyo bodi walijitahidi kuhakikisha kama vigezo hivyo wanavitumia, kwa wale 191 ambao wamepewa basi wamepita kwenye vigezo hivyo.

Kuhusu vigezo ambavyo vilitumika Mhe. Mwenyekiti naomba nivitaje kwa sababu suala hili la mkopo limekuwa ni tete kidogo na limezua mtafaruku mkubwa kidogo ndani ya nchi, hivyo kwa faida ya Baraza hili pamoja na Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vipao mbele ambavyo serikali kwa sasa ina wafanyakazi ambao tunawahitaji. Kwa hivyo, bodi yetu ilitizama vipaombele hivyo. Kwa mfano, kwa walimu tunalo tatizo la Walimu wa *Science, Geography, History* pamoja na *English*. Kwa upande wa *education* tulitumia vigezo hivyo.

Vile vile tunalo tatizo la wataalamu wa kilimo, uchumi, uhandisi pamoja na watu wengine kama hao Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, vipaombele vyetu tulilenga huko.

Lakini kwa wale wanafunzi ambao wamepata basi pia tuliangalia *points* zao. Kwa mfano, wale wa *Science* ambao waliopata kuanzia *points* 2.5 na kwa wale wa *Art* ni kuanzia *points* 5.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna wanafunzi ambao wanaoomba nafasi za kusoma kwenda nje, kwa kweli wanafunzi hao mara hii hatukuwatizama, kwa sababu mahitaji ya fedha ni makubwa. Kwa mfano, wanafunzi wanaoomba kwenda

kusoma Uingereza Mhe. Mwenyekiti, mwanafunzi mmoja anahitaji *Pound* elfu 999 sawa na milioni 20 za Tanzania.

Sasa bilioni 20 za Tanzania tunasomesha wanafunzi wanne katika vyuo ambavyo tunavyo na fani ile inapatikana ambayo mwanafunzi anataka kwende kusoma Uingereza. Kwa hivyo, suala hilo nalo pia liangaliwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna wanafunzi 111 hao ndio walioomba nje. Lakini kuna wanafunzi 223 wameomba fani za utawala na sheria, ambao wamesoma fani hizo hapa Zanzibar tunao wengi na bado hawajapata ajira, kwa hiyo hawa nao pia tumewaacha. *(Makofi)*

Jambo ninalotaka kumalizia katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, tunao *deal* nao ni wananchi ambao ni binadamu, kwa kweli binadamu anao udhaifu wake na wala siwezi kukataa moja kwa moja nikasema kwamba hakuna upendeleo au rushwa. *(Makofi)*

Lakini ikiwa Mhe. Mwakilishi anao ushahidi wa rushwa au upendeleo tena Mhe. Mjumbe yeyote, kwa sababu nyinyi ndio viongozi wa nchi hii, basi tunaomba utaratibu ufuatwe na tuletewe taarifa hizi rasmi kwenye wizara na tutazifanyiakazi na wala hatutamstahamilia mtu yeyote tena bila ya kulifumbia jicho suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, wizara yake ina mpango gani wa kutafuta mapato zaidi, ili wizara kuweza kuwasomesha waombaji wote wenye sifa za kuendelea na masomo hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nilieleza kwenye swali langu mama, kwamba bajeti ambayo tunapata kutoka serikalini ni ndogo na wala haikidhi mahitaji ya wanafunzi wetu, ambao wanataka kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Pamoja na mengi ambayo yamejitokeza, lakini uwezo wetu wa fedha ulikuwa ni mdogo, kwa kweli bajeti yetu ya mara hii ni bilioni 4 ndio ambayo ilipitishwa na Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi 1603 walihitaji zaidi ya bilioni 15.3, ili waweze kwenda kuendelea na masomo yao. Kwa hivyo, hili tumeliona na tunafikiria kutafuta njia mbadala ya bodi yetu kuwa na uwezo zaidi wa kifedha, kwa ajili ya kuwahudumia waombaji wetu.
Miongoni mwa mipango hiyo ni kuzungumza na mabenki, ambapo labda waombaji wetu ni wafanyakazi na hivyo benki ni wateja wao basi waweze kuwakopesha kwa mkopo ambao utakuwa hauna masharti makubwa. Vile vile kwa upande wa *ZSSF* wao hawa ni wateja wa wafanyakazi wetu, hivyo na wao tunazungumza nao, ili waweze kutukopesha.

Kwa upande wa wafanyabiashara ambao ni Wazanzibari wameonesha nia ya kuweza kutusaidia, basi tutawafuata hawa na kuwaomba watusaidie mkopo ambao hautokuwa na riba kubwa. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 14

Hospitlai ya Mnazimmoja Kuanzisha Huduma ya Bima ya Afya

Mhe. Mgeni Hassan Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa taasisi nyingi binafsi pamoja na mashirika mbali mbali yameanzisha Bima ya Afya, ili wafanyakazi wao waweze kupata huduma za afya kwa njia ya malipo. Kwa kuwa Hospitali ya Mnazimmoja ni hospitali pekee hapa Zanzibar yenye uwezo mkubwa wa kutoa huduma mbali mbali za afya.

(a) Je, ni lini Hospitali ya Mnazimmoja itaanza kuchukua wafanyakazi wenye bima?

(b) Je, serikali haioni kuwa kutokuwa na sera ya kupokea wafanyakazi wenye bima, kunainyima hospitali hiyo uwezo wa kuingiza mapato?

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazimmoja inaelewa umuhimu wa Bima ya Afya na kwamba hospitali hiyo imeanza kuchukua wafanyakazi wenye bima tangu tarehe 04/07/2008. Mashirika yaliofunga mkataba na Hospitali ya Mnazimmoja hadi sasa ni haya yafuatayo:-

(i) *National Health Insurance Fund of Tanzania (NHIF)*;
(ii) Mfuko wa Taifa wa Afya ya Jamii (*NSSF*);
(iii) Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*);
(iv) *Tanzania Revenue Authority (TRA)*;
(v) *Vendreda* (hawa ni jamaa wa *UN Agencies*) pamoja na
(vi) *Sogea Satom* hawa tumemaiza nao mkataba hivi karibuni.

Vile vile kuna mashirika mengine yaliyoonesha nia ya wafanyakazi kuhudumiwa na watafunga mkataba na Hospitali ya Mnazimmoja.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Sera yetu ya Uchangiaji iliyopitishwa mwaka 1999 na Baraza hili tukufu, inajumuisha Bima ya Afya. Malipo ya papo kwa papo na Mfuko wa Afya ya Jamii, yaani kule vijijini. Hivyo, upokeaji wa wafanyakazi wenye Bima ya Afya ni makubaliano kati ya taasisi husika na Hospitali ya Mnazimmoja tena kwa mkataba maalum.

Nam. 59

Uanachama wa *FIFA*

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa maombi ya Zanzibar kupata uanachama wa *FIFA* limeshakataliwa na kuondoa tama ya Wazanzibari kuwa wanachama wa taasisi hiyo kubwa ulimwenguni.

(a) Je, wizara inawaambia nini Wazanzibari kuhusu suala hilo?

(b) Kwa kukataliwa ombi letu hilo, wizara ina mipango gani ya kuishawishi tena *FIFA* kwa kushirikiana na *TFF*, *CECAFA* pamoja na *CAF*, ili Zanzibar ikubaliwe kuwa mwanachama wa *FIFA*?

(c) Je, wizara haioni kuwa ipo haja ya kushirikiana na Wizara ya Habari na Michezo ya Tanzania Bara kuishawishi *TFF* kuipatia mgao wa *FIFA, ZFA* unaotolewa kwa maendeleo ya mchezo huo kwa Watanzania kila mwaka, ili Wazanzibari wafaidike kwa kupata mgao huo wa *FIFA*?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 59 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hadi sasa ombi letu la kujiunga na FIFA limekataliwa kwa mujibu wa barua ya Katibu Mkuu wa FIFA ya tarehe 21/6/2011 Wizara imepokea kutoka Chama cha Soka cha Zanzibar (ZFA) shauri hili na tunapenda kuwaeleza wananchi kwamba huu ndio ukweli juu ya suali hili, aidha ni kawaida katika maombi unaweza kupata au kukosa, na kwa upande wetu, bahati haikuwa kwetu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa uzito na umuhimu wa uanachama wa FIFA kwa Zanzibar, Wizara na ZFA bado tunaendelea kushirikiana na taasisi husika kama vile TFF, CAF, CECAFA na FIFA yenyewe ili tuangalie uwezekano wa Zanzibar kupatiwa uanachama huo. Ni imani yetu kwamba bado tuna nafasi ya kulifuatilia suala hili pamoja na kurekebisha kasoro au utaratibu uliotumika hapo awali, sababu ya kukataliwa ombi letu ni kwamba kwa mujibu wa FIFA Zanzibar siyo nchi inayojitegemea na kutambulika Kimataifa.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ina imani kuwepo kwa umuhimu mkubwa wa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Tanzania Bara katika kutatua matatizo mbali mbali yanayoikabili ZFA kama vile ukosefu wa mgao huo katika FIFA pamoja na fursa nyengine. Aidha kwa kupitia Baraza la Michezo na ZFA wenyewe jitihada hizi tayari zinaendelea na tayari Kamati Maalum imeandaliwa na ZFA na inaendelea na kazi hiyo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na kusema ukweli wa hali ya mambo kuhusu ombi letu la FIFA, lakini hivi karibuni tu Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alifanya kikao maalum yeye na Rais wa TFF katika ukumbi wa VIP pale Bwawani, katika suala lililozungumzwa ni suala hili la uanachama wa FIFA.

Je, Mhe. Waziri ni makubaliano gani waliyokubaliana yeye na Rais wa TFF ili ule mgao wa FIFA unaotolewa kwa Tanzania katika kuendeleza mpira wa miguu kwa kuwapa mafunzo walimu wa mchezo huu, pamoja na kuendeleza mpira wa kinamama. Je, Zanzibar itafaidika vipi na mgao huo wa FIFA.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Naomba kutoa ufafanuzi zaidi juu ya maelezo ambayo ameyatoa Naibu Waziri ili kila mjumbe aondoke hapa iwe hana wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti kama inavyoeleweka kwamba juhudi kubwa zilichukuliwa kwa nguvu za pamoja kati ya ZFA, TFF na Serikali yenyewe ili kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo inakuwa ni miongoni mwa nchi wanachama wa FIFA, ukweli tulijenga tamaa kubwa na hasa tukizingatia kwamba tulipata ridhaa kutoka kwa Chama cha Mpira cha Tanzania cha TFF kwenyewe, lakini vile vile tukizingatia kwamba tulikizi masharti mengi ya FIFA na ukichukua kuna mifano mingine ya nchi kama zeti nchi kama England nao wana hali kama hiyo kuna Scotland, Wales na wao vile vile ni wanachama mbali wa FIFA.

Lakini kwa bahati mbaya suala hili hatimae lilikataliwa lakini pamoja na kukataliwa tulichukua hatua za kuwaita TFF na ZFA wakakaa pamoja ili kuona na kutafakari ili kuona kulikoni, lakini vile vile kubadilishana fikra ya nini tufanye ili tuhakikishe kwamba Zanzibar inabakia au nayo inapata fursa ya kuwa mwanachama wa FIFA.

Hakuna kitu kibaya kama kukataliwa na mkiamini kwamba kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi, kwa hivyo bado naamini kwamba bado iko fursa na iko tamaa ya Zanzibar kuwa mwanachama wa FIFA, kikao chetu nacho kimeamini hivyo. Kwa hivyo tumefikia pahala tukasema kwamba hili tufanye kama mbio za vijiti, imetoka kwenye michezo imeshindikana sasa imekuja kwenye kisiasa, kwa sababu za msingi Zanzibar imetolewa kwa sababu haina hadhi ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wajumbe naomba nichukue nafasi hii niseme kwamba hii ni fursa adhimu ya kuitumia, nyinyi ni wanasiasa na mimi ni mwanasiasa kwa hivyo hili suala limekuwa la kisiasa zaidi sio la kimichezo tena kwa sababu imeshindikanakwenye medani ya michezo, tuna fursa nzuri na wakati muafaka tuutumie wakati huu katika mabadilisho yetu ya katiba tuhakikishe kwamba Zanzibar angalau inapata ile *states* ya kimataifa angalau mashirikiano ya kimataifa ili tuweze kupata fursa ya kujiunga FIFA.

Mhe. Mwenyekiti, tulikaa na TFF na kutatua migogoro mingine vile vile juu ya mgao wa FIFA na kweli kulikuwa na matatizo, lakini hata hivyo tumefikia pahala kwamba sasa ZFA lazima ipate migao yake kama kawaida, kilichojiri hapa sio kwamba zinakuja fedha kinachozungumziwa hapa ni miradi. Kama vile kuwasomesha makocha, waamuzi hiyo ndio miradi yenyewe, kwa hivyo tumekubaliana kwamba TFF sasa itatoa miradi hiyo na itatoa pesa hizo kwa wakati ambao ZFA watahitaji.

Kwa hivyo waheshimiwa wajumbe nakuarifuni kwamba hakuna mgogoro tena kwenye TFF na hata hiyo ZFA yenyewe migogoro yote imeondoka, kwa hivyo waheshimiwa wajumbe kazi kwenu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa kamati yangu pia iliita vikundi vyote vya michezo na kwa kuwa ilikuwemo ZFA, kwa kuwa kamati yangu ililigusa suala hili na ikatoa maelekezo ambayo Wizara hii ingesaidia.

Je, atakubaliana nami Mhe. Waziri kwamba yale maelekezo tuliyoyatoa yachukuliwe haraka ili kuweza kuwa wanachama wa FIFA.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii: Hivi sasa tumo katika harakaati hizo za kuona yale yoto tuliyokusudia yanafanikiwa, hatua moja niliotoa nilisema ni kama mbio za vijiti, lazima tutumie fursa hii tuhakikishe kwamba Zanzibar nayo inapata ile *states ya* kimataifa, nafikiri hiyo ndio njia peke yake ambayo itaturuhusu sisi kuwa wanachama wa FIFA vyenginevyo tumegonga ukuta kwa njia za michezo hakuna njia huo ndio ukweli halisi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja fupi la nyongeza.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri amekuwa muwazi kueleza hali halisi ya ZFA kujiunga na FIFA, suala la ZFA kujiunga na FIFA halikuanza leo lilianza zamani tokea Mhe.Ali Juma Shamhuna alipokuwa Waziri wa wizara hii na Naibu Waziri Kiongozi, tulikuwa tukipewa maelekezo ya kutia moyo sana kwa wakati huo.

Lakini kwa sababu jibu lililotoka FIFA la mwazi wa nane mwaka huu kuhusiana na ombi hili, lili eleza kwamba barua namba mkwaju, TRE Mkwaju, PCO ambayo barua hii ilitiwa saidi na katibu wake, ilieleza kuwa Zanzibar wakati ni *state* ndani ya *state* na imepoteza utaifa wake haiwezi kuwa mwanachama wa FIFA kwa sababu ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini ukitizama kwa sababu mchakato huu umeanza zamani sana kulikuwa na Katiba ya Zanzibar ambayo ilikuwa ikieleza wazi kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, tukabadilisha katiba sasa tunasema Zanzibar ni Nchi, na hii katiba ya Jamhuri

ya Muungano inayotaka kufanyiwa marekebisho inasema Tanzania ni nchi moja, lakini sisi tunasema Zanzibar ni nchi na mipaka yake na kila kitu.

a) Ikiwa ni kujiunga na FIFA Tanganyika wao wamepoteza mpaka nchi na Zanzibar tuna nchi yetu, kwa nini zile haki zetu haziji huku huku wakati na hii ni nchi iliyoingia katika Muungano, badala yake zende kule Tanganyika iliyokuwa haipo.

b) Ni tatizo kubwa tena tatizo la kitaifa na lazima Zanzibar ilikomboe na ijulikane katika ulimwengu na wakati katiba yetu imeweka siku maalum ya kura ya maoni, kwa nini hatuitumii fursa hii tukawaambia wenzetu Wazanzibari wamo katika msimamo huu tukanyamaza kimya tu na kuridhika na hali inavyokwenda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Waheshimiwa Wajumbe mimi nafikiri tusiende mbali sana haya mambo ndio yameshatokea na hii ni miongoni mwa kasma hizo ambazo tunazungumzia katika masuala la muungano, ukweli katiba inasema hivyo lakini bado haijakidhi kimataifa ni ndani ya mipaka ya Tanzania hiyo inakubalika, lakini sasa ukitoka nje hali inakuwa nyengine, bado hatuna *state* za kimataifa lazima tukubali hilo.

Natoa wito tena fursa ni hii waheshimiwa wajumbe tuitumie na marakebisho ya katiba yanayokuja basi lazima tuhakikishe kwamba Zanzibar inapata *states* ya kimataifa hakuna jengine.

Nam. 44

Mahakama ya Ardhi

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kucheleweshwa kwa kesi/madai yanayohusiana na ardhi.

(b) Ikiwa eneo linalolalamikiwa ni la kilimo au biashara, na kwa kuwa shughuli zote katika eneo hilo husimama na kusubiri uamuzi; Mhe. Waziri haoni kuwa kulizuia eneo hilo kwa muda mrefu ni kurudisha nyuma shughuli za maendeleo katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 44 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu nyingi zinazopelekea kuchelewa kesi au madai, hata hivyo kwa sasa kesi za ardhi zimepungua kwa kiasi kikubwa baada ya

kuteuliwa Mahakimu wawili, mmoja Unguja na mwengine Pemba wanaoshughulikia mashauri yanayohusiana na ardhi. Hali halisi ya ardhi kwa Zanzibar ambapo kwa sasa ni chache na thamani yake ni imekuwa kubwa na shughuli za kiuchumi na kijamii zimeongezeka hali ambayo inaibua kesi nyingi za ardhi. Sababu ni kukosekana kwa taarifa muhimu kwa walalamikaji ambapo inakuwa vigumu kwa Jaji kuweza kutoa hukumu kwa haraka kutokana na kutopatikana kwa taarifa za umilikaji wa ardhi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kiutaratibu suala lolote linapopitia Mahakamani, Waziri hawezi kuliingilia, hivyo ucheleweshaji huo Waziri hana Mamlaka ya moja kwa moja ya kuingilia kati na kuilazimisha Mahakama kutoa hukumu.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala la nyongeza.

Kwa kuwa Mahakama ya Ardhi Pemba iko katika Ofisi ya Idara ya Ardhi Machomane Chake Chake tu. Je, ni lini Wizara yako kwa kufuatana na Wizara ya sheria na Katiba utafikiria kuanzisha mahakama ya ardhi Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kurahisisha ufikishwaji wa kesi za Kaskazini Pemba.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Kwa kuona kwamba kuna matatizo mengi ya masuala ya ardhi tumeongeza mahakimu Unguja na Pemba na kwa Pemba kuna Mahakimu wawili, mmoja atakuwepo Wete na mmoja atakuwepo Chake Chake, kwa hivyo suala la matatizo ya ardhi kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba limeshatatuliwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu waziri utakubaliana nami kuwa hizi kesi kwa kiasi kikubwa zinachingiwa na Wizara yenu kwa kutokufuata sheria za nchi hii, na kama utakaataa nitaomba nikuthibitishie Sheria namba 12 ya mwaka 1992 kifungu kidogo cha 55,56 naomba ukiangalie.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ikiwa mwenzetu anauliza suala na sisi ikiwa tutakuwa tunagonga huwa hatusikii wale yule anayeuliza masuala huwa hafahamu, tunaomba tumpe nafasi ili aulize suala lake kwa ufanisi na aweze kujibiwa kwa mujibu wa taratibu zilivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Mhe. Naibu waziri utakubaliana nami kuwa hizi kesi kwa kiasi kikubwa zinachingiwa na Wizara yenu kwa kutokufuata sheria za nchi hii, na kama utakaataa nitaomba nikuthibitishie Sheria namba 12 ya mwaka 1992 kifungu kidogo cha 55 na 56 naomba ukiangalie.

b) Hamuoni kuwa serikali mnaitia hasara kubwa kwa ufutaji viwanja kiholela na vibali vinavyotolewa nchi hii kisheria.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Si kweli kwamba Wizara ya Serikali ambacho ni chombo maalum cha serikali haifuati sheria za serikali, kwa sababu wizara hii hii inashiriki katika Baraza la Mapinduzi na katika baraza la Wawakilishi kuiandaa na kuipitisha sheria yote ya serikali, kwa hivyo kama mjumbe ana ushahidi kwamba kina kifungu cha serikali kimekiukwa akitaje ili tukifanyie uchunguzi.

Lakini amaagiza tuiangalie hiyo sheria nambari aliyoitaja tutaiangalia halafu tutajiuliza imekiukwa vipi sheria hiyo na hayo maamuzi yaliyowahi kutolewa wakati wowote.

Nam. 20

Serikali Kufufua Viwanda

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:

Hapo zamani kulikuwa na viwanda mbali mbali hapa Zanzibar vikiwemo viwanda vya mafuta ya nazi, sabuni, sigara n.k. Viwanda hivyo vilikuwa vikitoa nafasi kubwa ya ajira kwa vijana wetu. Kwa kuwa majengo ya viwanda hivyo bado japo kwa kuwa hakuna nafasi ya ajira ya kutoasha serikalini.

Je, Serikali hivi sasa haioni kuwa ipo haja ya kuvirudisha au kuvifufua viwanda hivi ili wananchi wapate ajira.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hapo zamani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa inamiliki na kuendesha viwanda vingi vilivyokuwa vikitoa ajira kwa wananchi. Lakini Serikali ilifanya maamuzi ya makusudi kujiondoa katika shughuli za uzalishaji na za biashara na kufungua milango ya fursa kwa wawekezaji kuekeza katika sekta hizo. Kwa hivyo Serikali ikauza vinwada vyake vingi na kukodisha vichache. Viwanda vya sabuni na mafuta ya nazi ni miongoni mwa viwanda vilivyouzwa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujikita katika uwekaji wa mazingira bora kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya sekta binafsi, ikiwemo miradi ya viwanda au kufufua viwanda vya zamani.

Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kupitia upya sera ya mwaka 1998 mpaka 19208 inayohusiana na sera za viwanda, tutaimarisha nguvu zote suala la *Microbes Small and Medium Enterprises* kuwashajihisha Wazanzibari wenye uwezo kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Katika sera hiyo tumeweka njia ya kutafuta *incentive* au vivutio maalum ambavyo vitavutia wawekezaji katika sekta ya viwanda, dhamiya ya Wizara yetu kuona kwamba viwenda vinashamiri ili kuwapatia ajira wananchi wetu na vile vile kuwapatia mapato serikali yetu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala la nyongeza kama ifuatavyo:

Je, atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba sasa iko haja ya kuviorodhesha viwanda vyetu vyote ambavyo havijauzwa, ili kuhakikisha kwamba ile kuuza uza kiholela ikomeshwe kuanzia sasa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Tangu kuingia katika Wizara hii navitafuta hivyo viwanda vidogo vidogo lakini sijaviona bado, lakini tuna makati maalum wa kuangalia kama kuna kiwanda kilichobakia au ghala iliyobakia ambayo kwamba haijauzwa tuitie katika orodha ya vitu vya serikali, mtu yoyote ambaye kuwa ana kiwanda au ghala bila ya hati ambayo ameuziwa tutamchukulia hatua kinidhamu ili kulikabidhi serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, jitihada hii imeshaanza tunapita katika maghala tukiona katika kumbu zetu hakuna tunamuita mwenye ghala na kumuuliza ghala hili umelipataje, *document* tuletee na kama hana tunamchukulia hatua. Kwa hivyo kazi hii imeshaanza na itaendelea kuona kwamba kila mali ya serikali ikiwa kiwanda ikiwa ghala ambayo iko chini ya Wizara ya Biashara. Viwanda na Masoko iliyokuwa haina hati inarejeshwa serikalini.

Vile vile naomba kutoa ahadi katika hadhara ya ukumbi huu kwamba kuanzia sasa Wizara yetu haitauza chochote kwa mtu yoyote, kwa sababu kuuza ni kutupa.

Nam. 95

Serikali Kuanzisha Mfumo Mmoja wa Mikopo ya Wananchi

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Pamoja na juhudi za kuanzisha mifuko ya JK na AK, wananchi wetu walio wengi hawakunufaika na mfuko huo. Aidha, kati ya wananchi wengi waliopata mkopo huo wanaamini kwamba fedha hizo wamepewa bure na hivyo hawalazimiki kulipa.

(a) Kwa lengo zuri la kuondosha kasoro zilizopo kati ya mifuko mingi inayoanzishwa hapa Zanzibar, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuanzisha Mfuko mmoja Mkuu *(Centralised Funds)* utakaohusika na mifuko yote hiyo, ili dhamira na malengo yake yakafahamika kwa wepesi kwa wanachi wetu.

(b) Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa kufuatilia mikopo inayotolewa katika Mifuko mbali mbali tunayoianzisha, Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha

mikopo yote iliyotolewa kwa wananchi inarejeshwa ili kuwanufaisha na wananchi wengine.

(c) Kuna sababu zipi zinazoikwaza Serikali kuweka Mfumo mmoja tu wa Mfuko kwa kila mikopo na dhamira nyengine za Mifuko inayoanzishwa katika kila awamu ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba umefika wakati tunahitaji kuupitia upya utaratibu wa mikopo mbali mbali ili kuweza kuleta ufanisi zaidi katika kusimamia utoaji na urejeshaji wa mikopo. Katika kufanikisha hili, Wizara yangu ina mpango wa kufanya tathmini juu ya taratibu za mikopo kupitia mifuko mbali mbali iliyopo hivi sasa ili kubaini mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto ambazo zitapaswa kushughulikiwa kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi. Aidha imeonekana kwamba kuna haja kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kuratibu mifuko hii ikiwa pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwa na Mfuko mmoja mkuu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi.

(b) Serikali imejipanga vizuri katika kuhakikisha mikopo inayotolewa kwa wananchi kupitia mifuko mbali mbali inarejeshwa ili kuwanufaisha na wananchi wengine. Mikakati iliyochukuliwa na Wizara yangu ni pamoja :-

(i) kuzishajihisha kamati za Uwezeshaji za Shehia na Wilaya zifanye kazi zake kama vilivyoainishwa kwenye muongozo wa Mpango wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

(ii) Kuwaelimisha wakopaji juu ya wajibu wao wa kulipa. Hii ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wateja kabla na baada ya kuchukua mikopo kuhusu taratibu za mikopo na suala zima la kusimamia vyema biashara zao ili ziweze kuwaletea tija na kuweza kulipa mikopo yao kwa wakati.

(iii) Kutoa taaluma kwa wanasiasa wabunge na wawakilishi ili wasaidie katika kutoa taaluma kwa wananchi kwani sauti zao zinakwenda mbali zaidi.

(iv) Kuwafuatilia wakopaji katika maeneo yao kwa kushirikiana na Masheha.

Aidha, Wizara imechukua hatua ya kupitia upya taratibu za mikopo na kuongeza vipengele katika muongozo wa usimamizi wa mikopo kwa lengo la kuimarisha utowaji na urejeshaji wa mikopo. Sambamba na hilo, mkataba wa mikopo nao pia unafanyiwa mapitio ili kuweka vipengele ambavyo vitasaidia kuwawajibisha zaidi wakopaji kurejesha mikopo kwa wakati.

(c) Kama nilivyoeleza katika majibu yangu kwenye kifungu (a), Serikali imepanga kuupitia upya utaratibu wa mikopo kupitia mifuko mbali mbali ili kuleta ufanisi na ikiwezekana kuwa na Mfuko mmoja tu mkuu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hata hivyo, hili litahitaji kufanyiwa kazi kwa umakini, ikiwemo kufanya utafiti utakaowezesha kupata taarifa zitakazosaidia kufanya uamuzi wa uhakika juu ya utaratibu utakaofaa zaidi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majbu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Waziri itakumbukwa kwamba Ofisi ya Waziri Kiongozi ya serikali ya awamu ya sita iliagiza gari ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itumike kwa sababu ya mfuko huo wa kujitegemea, mpaka sasa gari hiyo inatumika na Wizara ya Wanawake na Watoto je, kwa nini agizo hili hatukutekeleza kama tulivyoagizwa.

b) Kwa kuwa mfuko huu unakabiriwa na tatizo la ukosefu wa gari serikali haioni kuna haja gari hiyo kukabidhiwa kwenye bodi hiyo ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Ni kweli wakati kamati ilipokuja kwenye Wizara yetu pale ilitupa taarifa hiyo ya kwamba kuna gari hiyo ambayo ililetwa kwa ajili ya kazi ya mikopo, lakini hatimaye gari hiyo ikabakia katika Wizara ya Ustawi wa Jamii.

Gari ilikuwa ni mali ya serikali na Wizara inayotumia ni ya serikali, lililokuwepo sasa hivi ni sisi kujipanga vizuri tukatafuta utaratibu tukatumia gari ambayo au tukatafuta gari nyengine badala ya ile. Kwa sababu ile tayari sasa hivi imeshapangiwa kazi katika Wizara ya Ustawi wa Jamii ambayo ni ya serikali vile vile.

Lakini juhudi zinafanywa hivi sasa na ikiwezekana Mwenyezi Mungu akitujaalia katika kipindi kifupi kijacho tutafanya utaratibu tupate gari ambayo itasaidia kuziba pengo lile.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona tena. Naomba nimuulize Mhe. Waziri suala dogo tu la nyongeza. Katika majibu yake kakiri na kakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba mfumo unaofanyika hivi sasa una matatizo yake na haujaleta tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

Je, wizara ina mpango gani ya kuomba ushirikiano au msaada kutoka kwa nchi kama Bangladesh ambapo bwana Mohammed Yunus kwa kutumia. mfumo wa *Gramming Bank*, amefanikiwa sana kuwasaidia wananchi wa Bangladesh kutokana na umasikini kwa utaratibu wa mikopo ambayo inaonekana ina miongozo mizuri zaidi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Nilikuwa naomba arejee kidogo kuuliza hilo suali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Suala langu la nyongeza ni kwamba, kwa sababu katika majibu yake Mhe. Waziri amekiri na amekubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba utaratibu uliotumika hivi sasa hauonekana kuleta tija iliyokusudiwa pamoja na kukubaliana kuwa na mfuko mmoja kwa maana ya *Centralize Fund.*

Suala langu ni kwamba Wizara yake ina mpango gani wa kuona inaazima uzoefu wa nchi kama Bangladesh ambapo bwana Mohammed Yunus na *Gramming Bank* yake imefanikiwa sana kuwasaidia wananchi wa Banglandesh kuwapa mikopo ambayo imewaondoa katika umasikini kwa kiwango kizuri kabisa.

Wizara ina mpango gani wa kuazima mfumo kama huo wa Bangladesh wa kutumia mfumo wa *Gramming Bank* kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, wazo lake ni zuri na kama ni Wizara sisi tutakwenda na tutalisimamia. Sitaki kutumia neno tutakaa, kwa sababu ukilikalia haliji juu tena. Tutalisimamia suala hilo kuona kwamba tija hiyo ambayo imepatikana kwa upande huo basi na sisi tuhakikishe kwa upande na sisi inapatikana. Tukiona inaleta faida basi Ishalla tutakwenda katika utaratibu huo.

Mhe. Manajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba atakubaliana na mimi kwamba wananchi wengi hawana taaluma ya mikopo ile ya JK na AK na ndio sababu ya kushindwa kurejesha mikopo ile.

(a) Mhe. Waziri Wizara yako au serikali haiyoni kutoa taaluma kwanza na ndio mikopo ile ikatolewa.

(b) Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha mikopo iliyotolewa na kiasi gani cha mikopo iliyorejeshwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti , kwanza nakubali kwamba taaluma iliyotolewa haikufahamika vizuri. Hivi karibuni watendaji wa wizara yangu walifatilia wale ambao tuliwakopesha. Katika baadhi ya maeneo waliyokwenda walikiri wakasema kwamba mimi nashukuru Mungu mkopo ule wa Rais wetu wa AK na JK umenisaidia sana, kwa sababu ndio ulioniwezesha kuoa na watoto wawili walikuwepo pale nadhani kutokana na *product* hiyo.

Wengine wakasema kwamba tumeweza kutumia mikopo ile sisi mwanzo kwa sababu tuliona kama ni ruzuku kutokana na kwamba labda haikufahamika. Lakini sidhani kama kwamba haikufahamika moja kwa moja. Lakini labda utaratibu wa kuzitumia pesa zile haukutolewa vizuri. Kitakachofanyika hapa ambacho kinafanyika sasa hivi, tunatoa taaluma ya kutosha kwa wale ambao wanakopo juu ya utaratibu wa kukopa.

Nimesema hapa katika jibu langu kwamba tutafanya utaratibu maalum wa kutoa mafunzo kwa wale wote ambao wanakopo iwe mifuko ya AK mifuko ya JK iwe mifuko ambayo itaanzishwa mengine mipya, mifuko ya kujitegemea ni vyema kuhakikisha kwamba taaluma inatolewa. Tatizo kubwa lililokuwepo mtu unampa Shs. 50,000/- kama ni mkopo, unamtaka mwezi ujao aanze kulipa, mwananchi huyu yupo kijijini. Kutoka kule aje alipe Sh. 10,000/- benki, nauli ya kwenda na rudi inakaribia shs 5,000. *At the end* utaona kwamba anatumia mfuko wake. Kimsingi hapa inabidi tufanye utaratibu mzuri ili tuweze kuwa na watu kama wale wa wanaofanya sinema ya zamani Mobile Sine. Tuwe na maafisa wetu ambao wanatembea vijijini, wanakwenda kukusanya mikopo ile wao bila ya kuwasumbua wananchi kuleta huku mjini nadhani. Nadhani hiyo itawasaidia zaidi.

Kwa hivyo tunajaribu kutoa taaluma ili walipe huko huko walipo. Lakini pia tufikirie kuwapa nafasi ya kujiimarisha baada ya kuwapa mkopo tuwape kipindi kama cha mezi mmoja, miezi miwili halafu ndio tuanza kukusanya mikopo ile. Kwa hivyo ishaallah tutajitahidi kutua taaluma hiyo.

Mpaka sasa hivi pesa ambazo zimetolewa kwenye mifuko ile ya AK na JK ilikuwa karibu bilioni 1.4 na tayari benki zipo karibu bilioni 2.2, sasa hivi ambazo zinaratibiwa katika utoaji wa mkopo awamu ya pili. Kilichorejeshwa ni karibu milioni 450. Kwa hivyo kuna tatizo bado la urejeshaji kati ya bilioni 1.4 kilichorejeshwa kwa taarifa ambazo letes nilizozipata kuna na ongezeko la kama milioni 200 nyengine kutokana na taaluma tulizozitoa imesaidia kurejesha.

Mhe. Mwenyekiti, tumetumia mpaka mashekhe na aya za qur-an zimetumika katika kuwafahamisha wananchi wale ili waweze kurejesha. Kwa sababu ile ni amana wameichukua na inahitajiwa kurejeshwa. Ahsante sana.

Nam. 30

Tatizo la Mitaji kwa Wakulima na Wavuvi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza :-

Serikali imekuwa inatilia mkazo shughuli za kilimo na uvuvi kwa ajili ya kuinua vipato vya wananchi na kupunguza kazi ya umasikini nchini.

(a) Je, Mhe. Waziri anaelelewa kuwa tatizo kubwa la wananchi wengi wanaojishughulisha na uvuvi tatizo ni uwezo mdogo wa vitendea kazi na kukosa mitaji.

(b) Kama serikali inalielewa hilo, ina mpango gani wa kuwaondoshea wananchi tatizo hilo.

(c) Kwa nini serikali haianzishi Benki ya Maendeleo ya Wakulima na Wavuvi kama ni mpango maalum wa kuwaondolea wananchi tatizo la kukosekana kwa mitaji.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake Nam. 30 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Naelewa kwamba tatizo kubwa la wananchi wengi wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi na kilimo ni uwezo mdogo wa vitendea kazi na kukosa mitaji.

(b) Kwa kulielewa hilo serikali yetu imeanzisha Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Kiuchumi na Ushirika na kwa kweli inafanya kazi kubwa ya kuwaratibu namna ya kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi na baada ya muda mfupi matunda yake yataanza kuonekana kama ambavyo Mhe. Mwenyekiti mwenyewe punde amelijibu suala la Nam. 95.

(c) Serikali inayo azma na imo katika matayarisho ya uanzishwaji wa mifuko mbali mbali ya kutoa mikopo nafuu katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, ukiwa ni muelekeo ya hapo baadaye kuanzisha benki ya maendeleo ya sekta za kilimo, kwa lengo la kuwapa nafuu wananchi wetu katika kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwanza nikushukuru Mhe. Waziri kwa majibu yako mazuri kabisa nina masuala yangu mawili madogo tu ya nyongeza.

(a) Mhe. Waziri utakubaliana name kuwa hii ni kawaida yetu mawaziri kutujibu mko mbioni na hizo mbio sijui zinaanzia wapi na zitamalizikia wapi. Hayo matunda lini yatapeya ili wananchi waweze kufaidika.

(b) Utakubaliana nami kuwa asilimia 95 mpaka 98 ya Wazanzibari ni waislamu, huo mkopo nafuu utakuwa hauna riba. Na kama utakura na riba je, utakuwa si mtihani huo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Si kweli kwamba muda wote Mawaziri tunaposimama hapa tunasema serikali imo mbioni, kuna wakati mwengine huwa tunasema tumo katika mipango ya maandalizi na wakati mwengine tunasema tayari tumeshafanikiwa na wakati mwengine husema maneno mengine. Kwa hivyo asichukulie kwamba tunaposema kwamba tumo mbioni kwamba ni mara zote. Si kwali

(b) Benki ambayo itaanzishwa hapo baadaye serikali itashirikiana na wananchi na itachukua mawazo yao kabla ya kuianzisha kwa hivyo maoni ya wananchi yatazingatiwa ikiwa wananchi watasema hawataki riba basi hilo ndilo ambalo litakalochukuliwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kuuliza suali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa sababu Wizara yako imekusudia kuwanyanyua wavuvi ambao ni wavuvi wadogo wadogo na zana zao ni duni. Je, Wizara yako ina mpango gani au ina zana gani inazokusudia kuwapa wavuvi ili kuepukana na uvuvi duni walionao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, serikali imeanzisha mradi mkubwa unaotwa MIVARF *(Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Financing)* mradi huu unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili ambao jukumu lake kubwa ni kushughulikia mambo ya mitaji ya wananchi vijijini. Kwa hivyo shughuli za kilimo nazo zimo katika mpango wa mradi huu na ajiandae kuviimarisha vikundi vyake ili viweze kuwemo katika kufaidika na mradi huu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wengi wa jimbo langu la Wawi wamewekeza katika masuala ya kuvua na kwa kuwa serikali hadi leo hii bado hawajaweka utaratibu wa kuweka masoko ya kuuza bidhaa zao, hususan katika kipindi cha msimu ambapo samaki wanakuwa wengi katika soko, hilo huwapelekea kuuza samaki wao kwa bei ndogo sana na wanakuwa hawafaidiki.

(a) Je, ni lini serikali itatoa msaada kwa wale ili waweze kuyahifadhi mazao yale ya bahari na hatimaye kuyauza kwa bei katika msimu mwengine.
(b) Kwa kuwa serikali imeshaanza kupiga marufuku uvuvi wa kutumia bunduki katika jimbo langu. Anaweza akanieleza sababu za msingi za kuzuia uvuvi wa bunduki katika jimbo langu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba bidhaa za uvuvi zinakuwa na soko, serikali huwa inafanya mambo mengi. Kwanza ni kuhakikisha kwamba katika maeneo ya vijijini karibu na bahari, kunajengwa miundombinu ya masoko ili kwanza wavuvi wawe na maeneo mazuri ya kuuzia bidhaa zao. Lakini pia kuwepo na ghala au vifaa vya kuhifadhia samaki.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo la Wawi eneo karibu na Air Port serikali kupitia wizara yangu ilijenga soko suri pale Mvumoni lakini bahati mbaya hadi leo wananchi hawajataka kulitumia soko lile. Fedha nyingi zaidi ya milioni 30 zimepotea, mafiriza yamo pale jitihada kubwa zimefanywa lakini bado.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya kwanza watumie vile vifaa na miundombinu iliyowekwa pale ili kuona kwamba vinatumika vizuri na wateja wana eneo linaloeleweka la kuja kuchukua na kununua mazao ya wavuvi. Kuuza bidhaa katika maeneo ambayo siyo rasmi kwa

kweli hata wateja wanakuwa hawaelewi. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Mwakilishi ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya kuona miondombinu inayowekwa na wizara yangu kwanza inatumika. Ndio nia moja muhimu itakayoona kwamba wanaotaka bidhaa wana eneo ambalo linajulikana rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi wa kutumia bunduki na vioo huu ni uvivi ambao unaharibu sana mazingira yetu na sio tu unaharibu mazingira lakini pia unakausha *current stook* zilizomo baharini. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Mwakilishi awashajihishe wananchi wa jimbo lake kuona kwamba uvuvi huu tukiuendeleza basi utaleta matatizo makubwa, sio kwa wananchi wa jimbo la Wawi tu lakini kwa wananchi wote ambao wanatumia bahari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kumaliza kipindi cha Maswali na Majibu pana tangazo hapa.

Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanatakiwa mara tu baada ya kumaliza shughuli yetu ya leo hapa sote tuelekee Kilimani Zanzibar *Ocean View* kwa ajili ya Semina iliyoandaliwa na Afisi ya Rais na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi. Ahsante sana.

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa vile shughuli zetu za leo zimefikia hapa, nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hili hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 4:45 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi kesho
tarehe 20/10/2011 Saa 3:00 za asubuhi)